

‘RITA YAENDELEA KUFANYA MABORESHO YA MALIPO YA ADA KWA NJIA YA KIELEKRONIKI’

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) Umeanza utekelezaji wa malipo ya ada ya huduma zake zote kupitia mfumo mpya wa Serikali wa kielekroniki unaojulikana kama Government Electronic Payment Gateway (GePG) unaotumika katika Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali.

Akifunga Mafunzo ya siku tatu kuhusu mfumo wa malipo kwa njia ya kielekroniki yaliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango hii leo Jijini Dar es salaam, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson amesema mfumo huo wa malipo umepokelewa kwa mikono miwili na kwamba umekuja kutatua changamoto iliyokuwepo katika ofisi za Wakala zilizopo kwa Wakuu wa Wilaya Tanzania Bara ambapo hutegemea malipo kwa stakabadhi za Serikali zinazotolewa na Hazina na hivyo kupelekea baadhi ya maeneo kukumbwa na upungufu wa mara kwa mara.

“mfumo huu kwa hakika utaondoa changamoto hii ya kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi hasa kwa kipindi hiki ambapo Wananchi wengi wamekuwa uhitaji na uelewa juu ya huduma zetu ikiwemo ile ya usajili wa vizazi na vifo” alisema Bi Hudson.

Kwa upande wake Mkuu wa kitengo cha malipo kwa njia ya kielekroniki (GePG) kutoka Wizara ya Fedha na Mipango Bw Basil Baligumya amesema mfumo huu anatumika na taasisi kumi na tano (15) za Serikali na umeonesha mafanikio kwa kuongezeka uwajibikaji na uwazi katika ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa taarifa za kifedha kwa wakati pamoja na utoaji wa huduma kwa wakati kwenye Taasisi hizo za Umma.

Aidha ameongeza kuwa malengo ya Serikali ni kuona Taasisi zote za umma zinazohusika na ukusanyaji wa maduhuli zinaunganishwa katika mfumo huu wa malipo ya kielekroniki kwa lengo la kuongeza mapato na kuweka uwazi katika matumizi yake.

Tayari RITA Makao Makuu na Ofisi zake zote zilizopo kwa Wakuu wa Wilaya Jijini Dar es salaam zimeanza hii leo majaribio ya malipo ya ada zake kwa njia ya Mfumo mpya wa kielekroniki wa GePG na kisha baadaye kuusambaza katika Wilaya zote Tanzania bara.